




CHUO CHA UTAWALA WA UMMA  
S.L.P 1179  
TUNGUU – ZANZIBAR  
SIMU: +255242941210  
Email: [info@ipa.ac.tz](mailto:info@ipa.ac.tz)  
Website: [www.ipa.ac.tz](http://www.ipa.ac.tz)




**TANGAZO MAALUM KWA WIZARA, WAKALA, TAASISI  
ZINAZOJITEGEMEA NA MASHIRIKA YA UMMA YA SERIKALI YA  
MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar kinapenda kuzitaarifu Wizara, Wakala, Taasisi zinazojitegemea na Mashirika ya SMZ kuwa kinatarajia kuendesha mafunzo kwa watumishi wa Umma wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanaotarajiwa kustaafu.

Hivyo Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara, Mashirika na Taasisi za SMZ ambazo zina Watumishi wanaotarajiwa Kustaafu wanaombwa kuwasilisha orodha ya watumishi hao kwa Mkuu wa Chuo, Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar au kufika Chuoni Tunguu kwa upande wa Unguja au Tawi la Chuo cha Utawala wa Umma liliopo Jengo la zamani la (OR) Utumishi na Utawala Bora Chake Chake – Pemba. Mafunzo kwa Wastaafu watarajiwa yanatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 10 Machi, 2023.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nao kwa nambari zifuatazo: -

**Zantel:** +255 777 423 628. kwa upande wa Unguja na **Zantel:** 0777853125 kwa upande wa Pemba.”

  
**DKT. SHAABAN M. SULEIMAN,**  
**MKUU WA CHUO,**  
**CHUO CHA UTAWALA WA UMMA**  
**ZANZIBAR**

